TANGAZO LA SERIKALI NA. 776 la tarehe 18/9/2020

**SHERIA YA SERIKALI ZAMITAA (MAMLAKA ZA WILAYA), (SURA YA 287)**

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153(1))*

**SHERIA NDOGO ZA (UDHIBITI WA BIASHARA YA MAZAO YA MISITU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE ZA MWAKA, 2020**

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe za Mwaka 2020.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo: -

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Njombe;

"Mazao ya Misitu" maana yake ni mbao, nguzo ndogo (Milunda), nguzo kubwa, mkaa, magome ya miti, fito, na magogo mabichi na makavu;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, na ni pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika ambalo linanunua mazao ya Misitu ndani ya Halmashauri na itahusisha pia mtu, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi au Shirika ambalo linasafirisha mazao nje ya Halmashauri;

"Muuzaji" maana yake mtu, Kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi au shirika lolote linalojishughulisha na uzalishaji au uuzaji wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri;

"Serikali ya kijiji" maana yake ni mamlaka ya kijiji iliyopo ndani ya mamlaka ya Halmashauri na ambapo biashara ya mazao ya misitu inafanyika;

"Ushuru" maana yake ni ushuru wa mazao ya misitu usiozidi asilimia 5 ya bei ya kununulia mazao ya misitu unaolipwa na mnunuzi kwa Halmashauri;

"Ushuru wa huduma" maana yake ni ushuru wa huduma unaolipwa kwa Halmashauri na muuzaji wa mazao ya misitu kutokana na asilimia 0.3 ya mauzo ya biashara husika;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, Kampuni, Taasisi, Shirika au Serikali ya Kijiji atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Uanzishaji wa utaratibu maalum wa uuzaji na ununuziwa mazao ya misitu

4. (1) Halmashauri itaanzisha utaratibu maalumu wa uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu yanayopatikana ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(2) Mazao ya misitu yatauzwa, kununuliwa na kutozwa bei kwa kutumia kipimo cha mita za ujazo.

(3) Kila muuzaji na mnunuzi wa mazao ya misitu anawajibika kuuza au kununua mazao ya misitu na kutoza bei ya zao husika kwa kutumia kipimo cha mita za ujazo.

Maeneo ya kuuza na

5. (1) Halmashauri itanzisha masoko maalumu ya kuuza na

kukaushia mbao

kununua mbao.

(2) Mbao zitakaushwa, kuuzwa na kununuliwa kwenye maeneo maalumu yaliyoidhinishwa na Halmashauri kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi

(3) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kuuza, kununua, kuanika au kukausha mbao kwenye maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.

Wajibu wa mnunuzi wa mazao ya misitu

6. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya eneo kununua mazao na kulipa malipo kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo kwa kila zao atakalonunua ikiwa ni pamoja na kulipa ushuru unaostahili kwa Halmashauri.

(2) Itakuwa ni kosa kwa Mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri kununua mazao ya misitu kinyume na utaratibu ulioelezwa katika kifungu cha kwanza.

Wajibu wa muuzaji wa mazao ya misitu

7. (1) Itakuwa ni wajibu wa kila muuzaji wa mazao ya misitu kuuza na kutoza bei ya mazao yake ya misitu kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo ikiwa ni pamoja na kulipa ushuru unaostahili kwa Halmashauri.

(2) Itakuwa ni kosa kwa muuzaji wa mazao ya misitu kuuza na kutolipa ushuru unaostahili kinyume na utaratibu ulioelekezwa katika kifungu cha kwanza.

Leseni ya biashara ya mazao ya misitu

8. (1) Kila Muuzaji wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri atalazimika kuwa na leseni ya kuendesha biashara ya mazao ya misitu.

(2) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, leseni ya usajili wa biashara ya mazao ya misitu itakuwa ni lazima kwa kila muuzaji wa mazao ya misitu ikiwa ni pamoja na mtu yeyote anayeuza mazao hayo kutoka

shambani kwake.

(3) Ni kosa kwa Muuzaji yeyote wa mazao ya misitu kuendesha biashara ya mazao ya misitu bila kuwa na leseni ya usajili wabiashara ya mazao ya misitu na leseni ya biashara ya mazao ya misitu kutoka Halmashauri.

Wajibu wa kulipa Ushuru wa Huduma na Ushuru wa mazao ya Misitu

9. (1) Itakuwa ni wajibu kwa kila muuzaji wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri kulipa ushuru wa huduma.

(2) Ushuru wa mazao ya misitu utakaolipwa kwa Halmashauri kwa mujibu wa kifungu cha (1),ni kutokana na muuzaji kuendesha biashara ya mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri kulipa ushuru wa mazao ya misitu usiozidi asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia.

(4) Katika kudhibiti ukwepaji wa ulipaji ushuru wa mazao ya misitu, bei ya soko ya wakati huo itatumika katika kukokotoa ushuru anaotakiwa kulipa Mnunuzi wa mazao ya misitu.

(5) Ushuru wa mazao ya misitu utalipwa kwa afisa mwidhiniwa au waka na kupewa stakabadhi ya Halmashauri kabla ya mnunuzi wa mazao kusafirisha mazao husika.

Vibali vya kuvuna, kuuza na kununua mazao ya misitu

10. (1) Utakuwa ni wajibu wa kila Serikali ya Kijiji ndani ya mamlaka ya Halmashauri kuhakikisha inatoa vibali vya uvunaji, uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu kwa kila mvunaji muuzaji, na mnunuzi ndani ya Kijiji husika.

(2) Utaratibu wa utoaji wa vibali vya uvunaji, uuzaji, upakiaji na ununuzi wa mazao ya misitu ndani ya kijiji utakuwa ni wa lazima kwa kila muuzaji na mnunuzi.

(3) Kila mvunaji, muuzaji na mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya Kijiji atalazimika kupata kibali cha uvunaji,uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu katika Ofisi ya Kijiji kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

(4) Serikali ya Kijiji inaweza kufuatilia na kujiridhisha endapo muuzaji au mnunuzi wa mazao ya misitu aliyepewa kibali cha ukataji au ununuzi wa mazao ya misitu anazingatia matakwa ya Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa wakala au afisa mwidhiniwa

11. (1) Halmashauri inaweza kumteua wakala au afisa mwidhiniwa kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala au Afisa mwidhiniwa atakayeteuliwa na Halmashauri atakuwa na jukumu la kuhakikisha matakwa ya Sheria Ndogo hizi yanatekelezwa na kutoza faini kwa niaba ya Halmashauri kama ilivyoelezwa na Sheria Ndogo hizi.

Viwango vya bei za uuzaji mazao

12. (1) Bila ya kuathiri masharti yoyote ya Sheria Ndogo hizi, bei za uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu itatozwa kwa kipimo cha mita za ujazo kwa kila aina ya zao la msitu.

(2) Bei ya uuzaji na ununuzi wa kila zao la misitu itatozwa kulingana na hali halisi ya soko la mazao ya misitu kwa wakati huo.

(3) Bila kuathiri masharti yaliyotajwa katika kifungu cha (1) na (2) hapo juu, Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali Kuu na vyama vya wakulima wa miti inaweza kutoa bei elekezi ya uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri bila kumwathiri muuzaji na mnunuzi wa zao husika.

Uanzishwaji wa vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu

13. (1) Halmashauri inaweza kuanzisha vituo mbalimbali ndani ya Halmashauri kwa madhumuni ya kukagua mazao ya misitu yanayosafirishwa kutoka ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(2) Ukaguzi wa mazao ya misitu katika vituo utahusisha uhakiki wa nyaraka za uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu, ushuru uliolipwa, bei ya kununulia na vibali vilivyotolewa kijijini kuruhusu uuzaji na ununuzi wa mazao ya misitu.

Usafirishaji wa mazao ya misitu

14. (1) Kila msafirishaji wa mazao ya misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri atahakikisha anapata nyaraka muhimu za kusafirisha mazao ya misitu kama ifuatavyo -

a) kibali vya uvunaji wa mazao ya misitu vilivyotolewa na Kijiji kwa muuzaji na mnunuzi wa zao hilo;
b) kibali vya upakiaji;
c) nyaraka zinazoonyesha bei iliyotumika kununua zao husika kwa vipimo vya mita za ujazo;
d) kibali cha kusafirisha zao husika;
e) nakala ya stakabadhi ya ushuru uliolipwa na muuzaji au mnunuzi wa mazao hayo;
f) leseni ya usajili wa biashara ya mazao ya misitu; na
g) leseni ya biashara ya mazao ya misitu kutoka Halmashauri.

Muda wa kupakia na kusafirisha mazao ya misitu

15. (1) Muda wa kupakia mazao ya misitu utakuwa ni kati ya saa 12:00 asubuhi na saa 12:00 jioni.

(2) Muda wa kusafirisha mazao ya misitu itakuwa ni kati ya saa 12:00 asubuhi na saa 12:00 jioni na si zaidi ya hapo.

(3) Upakiaji na usafirishajiwa mazao ya misitu unaweza kufanyika usiku iwapo msafirishaji atakuwa amepata

kibali maalum cha kusafirisha mazao ya misitu usiku kutoka kwa afisa mwidhiniwa.

(4) Itakuwa ni kosa kwa msafirishaji yeyote wa zao la misitu ndani ya mamlaka ya Halmashauri kusafirisha mazao ya misitu bila kuzingatia masharti ya kifungu hiki.

Kutaifisha Mazao ya misitu

16. (1) Baada ya kupata kibali cha Mahakama Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kutaifisha na kuuza mazao ya misitu yaliyouzwa au kununuliwa bila kufuata masharti ya Sheria Ndogo hizi iwapo mwenye mazao hayo ya misitu ametoroka na kuyatelekeza.

(2) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea kwa muuzaji au mnunuzi wa mazao ya misitu yaliyotaifishwa, kwa kutekeleza mamlaka yake ya kuuza mazao hayo,isipokuwa kama hasara hiyo imesababishwa na uzembe wa Halmashauri.

Kufililisha makosa

17. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha makosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum na kulipa ada au ushuru anaodaiwa kama iliyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

Makosa

18. Mtu yoyote atakuwa ametenda kosa endapo-

a) atauza mazao ya misitu kinyume na Sheria Ndogo hizi;
b) atanunua mazao ya misitu kinyume na Sheria Ndogo hizi;
c) atasafirisha mazao ya misitu bila ya kuwa na nyaraka zilizoelezwa katika Sheria Ndogo hizi;
d) atamshawishi mtu au kundi la watu kukiuka matakwa ya Sheria Ndogo hizi;
e) atakataa au kushindwa kutii maagizo halali ya afisa mwidhiniwa au wakala;
f) atamzuia afisa mwidhiniwa au wakala

kutekeleza majukumu yake;

g) atalazimisha kupita katika vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu kwa nguvu bila kukaguliwa;

h) ataendesha biashara ya mazao ya misitu bila kuwa na leseni ya usajili wa biashara husika;

i) ataendesha biashara ya mazao ya misitu bila kuwa na leseni ya biashara kutoka Halmashauri;

j) atauza mazao ya misitu bila kulipa ushuru wa Halmashauri;

k) atanunua, kuuza au kutorosha mazao ya misitu kwa madhumuni ya kukwepa masharti ya Sheria Ndogo hizi; na

l) atasafirisha mazao ya misitu nyakati za usiku bila kibali maalum.

Adhabu

19. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na endapo akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo kwa pamoja.

## JEDWALI LA KWANZA

*(chini ya kifungu cha 5(2)*

## MASOKO NA MAENEO YA KUKAUSHIA, KUUZA NA KUNUNUA MBAO

1. Idamba
2. Igongolo
3. Ikondo
4. Ikuna
5. Kichiwa
6. Kidegembye
7. Lupembe
8. Matembwe
9. Mfriga
10. Mtwango
11. Nyombo
12. Ukalawa

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 10(3))*

FOMU NAMBA 1

SHERIA NDOGO (UDHIBITI WA BIASHARA YA MAZAO YA MISITU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE ZA MWAKA, 2020

KIBALI CHA KUVUNA/KUUZA MAZAO YA MISITU KATIK HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

1. Jina mvunaji/muuzaji:_______________________________________
2. Anuani S.L.P_____mji/kijiji______kitongoji_______ Simu_______
3. Mahali anapoishi Mji/Kijiji _________ Kitongoji:______________
4. Aina ya zao analotaka kukata:_______________________________
5. Jina la Mnunuzi:_________________Anuani__________________
6. Kiasi cha mazao kichovunwa/uzwa:___________________________
7. Namba ya leseni ya biashara ya mazao ya misitu________________

MIMI_______________________________________NAAPA / NATHIBITISHA kwamba nitauza mazao yangu ya misitu kwa kuzingatia matakwa ya Sheria Ndogo (Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Misitu) za halmashauri ya Wilaya ya Njombe za Mwaka, 2020 kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo katika kutoza bei na sio Vinginevyo. Pia natambua kuwa kuuza mazao hayo kinyume na matakwa ya Sheria Ndogo hizi ni kosa na nastahili adhabu.

Tarehe ya kuomba kibali: _______________________________________

Saini ya Mwombaji:___________________________________________

Tarehe ya kutolewa kibali:______________________________________

Jina la Afisa Mtendaji waKijiji__________________________________

Saini ya Afisa Mtendaji:________________________________________

Mhuri wa Mtendaji wa Kijiji:____________________________________

FOMU NAMBA 2

KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO YA MISITU KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

1. Jina la Mnunuzi:________________________________________
2. Anuani S.L.P _____ Mji/kijji _____ kitongoji_____ Simu ______________
3. Aina ya zao analotaka kununua:____________________________
4. Jina la Muuzaji:___________
5. anuwani __________________
6. Kiasi cha Mazao ya misitu kitachonunuliwa:_________________________

MIMI_______________________________________NAAPA / NATHIBITISHA; kwamba nitanunua mazao ya misitu kwa kuzingatia matakwa ya Sheria Ndogo ( Udhibiti wa Biashara ya Mazao ya Misitu) za Halmashauri ya Wilaya ya Njombe za Mwaka 2020 kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo katika kulipa bei na sio Vinginevyo. Pia natambua kuwa kununua mazao hayo kinyume na matakwa ya Sheria Ndogo hizi ni kosa na nastahili adhabu.

Tarehe ya kuomba kibali: ____________________________________

Saini ya Mwombaji:_________________________________________

Tarehe ya kutolewa kibali:____________________________________

Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji:_______________________________

Saini ya Afisa Mtendaji:_____________________________________

Mhuri wa Mtendaji wa Kijiji:__________________________________

JEDWALI LA TATU
*(Limetungwa chini ya kifungu cha (17)*

HATI YA KUFILILILISHA MAKOSA

Mimi ………………………………………… nakiri KWA HIYARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Njombe, kwamba tarehe …… ya mwezi ………………. mwaka ………………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …………………………… cha Sheria Ndogo za (Uthibiti wa Biashara za Mazao ya Misitu) za Wilaya ya Njombe za Mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, niko tayari kulipa faini ya kiasi cha shilingi laki mbili pamoja na ada au ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO NILIYOTOA HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………. ya mwezi……… mwaka ……………………….
Jina…………………………………… Saini………………..……………

Mbele ya:
Jina: ……………………………………………
Cheo: …………………………………..……….
Saini: ……………………….….………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililotolewa katika kikao cha baraza la madiwani cha tarehe 31 /7/2019 na kushuhudiwa na:

…………………………………
ALLY J. ALLY
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.*

……………………………………..
VALENTINO A. HONGOLI
*Mwenyekiti wa Halmshauri*
*Halmashauri ya Wilaya ya Njombe*.

**NAKUBALI**

Dodoma,
1st September, 2020

………………………………
SELEMANI S. JAFO (MB)
Waziri wa Nchi-0R-TAMISMI